# ARDHI N UHAI

HAKIARDHI ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 12 MEI - AGOSTI 2014

## UWEKEZAJI MKUBWA CHACHU YA MIGOGORO YA ARDHI VIJIJINI?

*Licha ya kuainishwa kwa taratibu za uwekezaji kisheria, kumekuwa na migogoro baina ya makundi mbalimbali hasa kutokana na ukiukwaji wa taratibu za usimamizi na mgawanyo wa ardhi usiozingatia maslahi ya makundi yote yanayotumia rasilimali husika.*

*Na; Alice Shamge*



*Shamba la mwekezaji wa Chai Mufindi*

Katika miaka ya hivi karibuni nchini Tanzania kumekuwa na wimbi la uwekezaji mkubwa katika ardhi ya vijiji ambapo wawekezaji wa ndani na nje huwekeza katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa mazao ya chakula na ya biashara kama vile jatropha, mahindi, mpunga, miti pamoja na uchimbaji wa madini.

Uwekezaji ni suala linaloainishwa kwa mujibu wa sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 1997 inayoruhusu mwekezaji kutoka nje kuomba ardhi kupitia Kituo cha Uwekezaji nchini na kumilikishwa kwa hati hafifu inayotolewa na kituo hicho.Wawekezaji wa ndani wanaweza kupata ardhi kufuata taratibu za kawaida za umiliki wa ardhi nchini. Licha ya kuainishwa kwa taratibu za uwekezaji kisheria, kumekuwa na migogoro baina ya makundi mbalimbali hasa kutokana na ukiukwaji wa taratibu za usimamizi na mgawanyo wa ardhi usiozingatia maslahi

*Inaendelea uk. 3* »

YALIYOMO


- Uwekezaji mkubwa chachu ya migogoro ya ardhi vijijini 1-3
- Athari za upanuzi wa maeneo ya hifadhi za wanyamapori 1- 4
- Mpango wa matumizi ya ardhi 5
- Migogoro ya ardhi inahitaji suluhu ya kudumu 6
- Maoni ya mwananchi 7
- Utatuzi wa migogoro 8
- Ugunduzi wa gesi chachu ya maendeleo 10


## ATHARI ZA UPANUZI WA MAENEOYA HIFADHI ZA WANYAMAPORI KWA WAKAZI WA MAENEO JIRANI.


*Na; Valentin Ngorisa Olyang'iri*

Ujumbe mkuu katika makala hii ni kuwa, historia ya upanuzi wa maeneo ya hifadhi za wanyamapori nchini Tanzania imejaa simulizi za kukatisha tamaa sana juu ya ukatili na ukiukwaji mkubwa wa haki kwa wananchi waliobahatika kuishi katika maeneo ya hifadhi au jirani na hifadhi hizo. Vipigo vya askari wa wanyamapori, unyanyasaji wa kijinsia, kuchomewa makazi, mazao na mali, kujeruhiwa na kusababishiwa ulemavu wa kudumu, ni baadhi tu ya madhila ambayo wananchi wa Ngorogongoro, Serengeti, Selou na kwingineko kwenye hifadhi za wanyama pori wamekuwa wakikabiliana navyo tangu kuanzishwa kwa hifadhi hizo.

Historia ya uhifadhi nchini Tanzania ilianza tangu wakati wa ukoloni wa Wajerumani na Waingereza walipoanzishwa mapori ya akiba ya Selous, Serengeti na Ngorongoro kwenye miaka ya 1920. Mwaka 1959 serikali ya kikoloni ya Kiingereza iliitangaza Serengeti kuwa hifadhi rasmi na kuwatenganisha rasmi

*ni jukumu letu sote kuhakikisha kuwa wanyamapori na mapori yao yanalindwa kwaajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.*

*Inaendelea uk. 4* »




**ARDHI NI UHAI** Ni jarida la Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI) ambalo hutolewa mara tatu kwa mwaka.

Kusudi kubwa ni kuwapa wadau wa Taasisi hii taarifa mbalimbali zinazohusiana na mambo ya ardhi

**MHARIRI**
Yefred Myenzi

**BODI YA WAHARIRI**

| | | |
|---|---|---|
| Ng'wanza Kamata | - | M/Kiti |
| Abdallah Matata | - | Mjumbe |
| Rehema Mfaume | - | Mjumbe |
| Alice Shamge | - | Mjumbe |
| Mchapishaji | - | HAKIARDHI |
| Mchapaji | - | iPrint |
| Msanifu | - | Arnold Njuki |

**UJUMBE WA BODI KWA WASOMAJI**
WASOMAJI wa jarida hili nakaribishwa kutoa michango yenu kwa kuuliza maswali, kutoa ushauri, maoni, au kwa kuandika makala (zisizozidi kurasa tatu) kwa mhariri kupitia anuani zifuatazo:

HAKIARDHI
*Land Rights Research & Resources Institute*

Kitalu No.236 Block 47 Sinza Mori, Mkabala na Wanyama Hotel, S.L.P 75885, Dar es Salaam
Simu +255 22 2771360/ 0784 646752,
Nukushi: +255 22 2771362
Baruapepe: info@hakiardhi.org,
Tovuti: www.hakiardhi.org





# Ushiriki wa wananchi utaepusha migogoro ya ardhi nchini

*Migogoro mingi inatokana na kutowashirikisha wananchi kikamilifu katika maamuzi yanayohusu utoaji wa ardhi kwa uwekezaji husika.*

Migogoro ya ardhi imeendelea kuyagusa maisha ya wazalishaji wadogo hususan wanaotumia na kuitegemea ardhi kujikimu na kuendesha maisha yao. Kwa takribani miaka mitano mfululizo tangu mwaka 2010, wizara ya ardhi imekuwa ikieleza katika hotuba zake za bajeti kuwa migogoro hii imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka huku kasi ya uanzishwaji wa mabaraza na mahakama za utatuzi ikiwa ndogo sana kwa mwaka. Ni dhahiri kwamba, ongezeko hili la migogoro linahusishwa na sababu nyingi lakini hatuwezi kuacha kuhusisha moja kwa moja na ongezeko la uwekezaji mkubwa kwenye ardhi za vijiji.

Hivi karibuni, Tanzania imeshuhudia uwekezaji mkubwa katika maeneo matano muhimu. Kwanza, kilimo cha mazao ya nishati mimea kama jatropha, michikichi na miwa kwa ajili ya kutengeneza mafuta ya mitambo na kusafiria yenye kiwango kidogo cha hewa ya ukaa. Pili, yapo makampuni yanayowekeza katika mazao ya chakula kwa ajili ya kuuza nje ya nchi. Tatu, kuna uwekezaji katika uchimbaji wa madini na gesi asilia. Nne, uwekezaji katika upandaji wa misitu ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na eneo la tano ni upanukaji wa hifadhi za wanyamapori kwa malengo ya kupanua biashara za utalii.

> MASLAHI YA WANANCHI NI KUENDELEA KUJIKIMU KUTOKANA NA RASILIMALI HUSIKA NA KUMUDU HUDUMA NYINGIE ZA KIJAMII.

Pamoja na manufaa mengi yanayoweza kupatikana kutokana na uwekezaji katika sekta zote hizo, bado jamii zinazozungukwa na uwekezaji zimejikuta zikikabiliwa na wimbi la migogoro inayohusisha matumizi ya ardhi iliyotolewa au kuchukuliwa kwa ajili ya uwekezaji. Migogoro mingi inatokana na kutowashirikisha wananchi kikamilifu katika maamuzi yanayohusu utoaji wa ardhi kwa uwekezaji husika. Ipo mifano hai kutoka Loliondo, Kahama, Rufiji, Kilwa, Mpanda, Mbarali na hivi karibuni Mtwara ambako wananchi wamejikuta katika wakati mgumu wakitakiwa ama kuachia maeneo yao au kuondoshwa kwa nguvu kupisha uwekezaji.

Ni mawazo yetu kuwa ushirikishwaji wa wananchi utawapa nafasi ya kuelewa manufaa na athari zinazotokana na uwekezaji husika na hivyo kufanya maamuzi sahihi ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima. Kijijini ni mahali ambapo demokrasia ya kweli bado inawezekana kwa kila mwananchi kushiriki kwenye maamuzi kwa njia ya vikao halali hususan vya mkutano mkuu wa kijiji. Wananchi walioshirikishwa, wana nafasi ya kuhoji, kudadisi, kukubaliana na hata kukataa uwekezaji wa aina fulani hasa pale watakapobaini kuwa hauendani na matakwa wala maslahi yao. Maslahi ya wananchi ni kuendelea kujikimu kutokana na rasilimali husika na kumudu huduma nyingie za kijamii. Ni wakati wa kufanya maamuzi yanayohusisha wananchi wenyewe.

**Yefred Myenzi**
**MHARIRI**

» Inatoka uk. 1

# UWEKEZAJI MKUBWA CHACHU YA MIGOGORO YA ARDHI VIJIJINI?

ya makundi yote yanayotumia rasilimali husika. Baadhi ya watu wanavamia maeneo yasiyokuwa yao kwa kisingizio cha uwekezaji bila kuzingatia sheria na haki za raia. Kundi hili la wavamizi linahusisha wageni na wenyeji pia lakini kwa kusaidiwa na baadhi ya watendaji wa vijiji, kata na Wilaya wasiozingatia maadili ya kazi zao.

Sababu nyingine ni kukosekana kwa uelewa wa wanavijiji kuhusu taratibu za uwekezaji. Wawekezaji wajanja hutumia fursa hii kuwarubuni wananchi hao, na hivyo kujikuta wanaidhinisha kutolewa kwa eneo kwa ajili ya uwekezaji bila kujua athari zake. Wakati mwingine wawekezaji wamehusishwa na tuhuma za kuwarubuni wananchi kwa kupitia viongozi wa serikali za vijiji wenye uchu wa fedha kupata ardhi isivyo halali. Mara nyingine katika Mkutano Mkuu wa Kijiji akidi haifikiwi lakini viongozi hawa huorodhesha majina na idadi ya uongo kwa kuchukua mahudhurio ya mikutano mingine isiyohusiana na ugawaji ardhi kwa mwekezaji. Baadae wananchi wakigundua kuwa wamekosea, inakuwa vigumu kubadilisha maamuzi na hivyo kukosa ardhi moja kwa moja.

MARA NYINGINE KATIKA MKUTANO MKUU WA KIJIJI AKIDI HAIFIKIWI LAKINI VIONGOZI HAWA HUORODHESHA MAJINA NA IDADI YA UONGO KWA KUCHUKUA MAHUDHURIO YA MIKUTANO MINGINE ISIYOHUSIANA NA UGAWAJI ARDHI KWA MWEKEZAJI.

Aidha, wananchi wengi hawaelewi tofauti ya hekta na ekari hali inayosababisha kugawa ardhi kubwa bila kujua ukubwa wa eneo walilotoa. Hekta moja ina ukubwa wa ekari mbili na nusu lakini wananchi wengi wanafikiri vipimo hivyo viko sawa. Mifano michache hapa chini inajaribu kufafanua maelezo ya hapo juu.

Katika Wilaya ya Hanang ubinafsishaji wa mashamba ya ngano yaliyokuwa chini ya shirika la Kilimo na chakula NAFCO umekuwa na migogoro isiyoisha. Mwaka 2006, serikali iliamua kurudisha mashamba mawili ya Warret na Gawal kwa wananchi wa maeneo husika kati ya mashamba saba yaliyokuwa chini ya NAFCO. Hata hivyo, mgawanyo wa mashamba hayo kati ya wakulima na wafugaji ukaingiliwa na siasa za makundi na vitendo vya rushwa kiasi cha kukwamisha mchakato mzima. Hatimaye baadhi ya wananchi wamebahatika kupata maeneo ya malisho na wengine kilimo lakini kwa gharama za kuyalinda kwa mishale na mikuki na kutishia uhai wa makundi mengine.

Eneo jingine ambalo limekuwa na migogoro mingi kutokana na uwekezaji ni wilaya ya Mbarali kwenye shamba la mpunga Kapunga ambapo mwekezaji alimilikishwa eneo kubwa linalochukua hadi maeneo ya wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba hilo. Mgogoro umedumu tangu mwaka 2006 shamba hili lilipobinafsishwa. Jumla ya hekta 1,870, zimemilikishwa kwa mwekezaji ambazo zilikuwa sehemu ya ardhi ya wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba hilo. Matokeo yake mwekezaji hutumia sehemu tu ya eneo na kukodisha sehemu kubwa ya shamba kwa wananchi jambo ambao ni kinyume taratibu za uwekezaji.

Mfano mwingine ni Makampuni yanayoshughulika na kilimo cha nishati uoto yaliyowekeza Kisarawe, Bagamoyo, Lindi na maeneo mengine ya ukanda wa pwani. Kampuni ya Bioshape yenye asili ya Uholanzi ilipata kiasi cha hekta 34,000 za ardhi wilayani Kilw. Badala ya kujihusisha na ulimaji wa jatropha kama ilivyokusudia iliamua kufyeka misitu na kuanzisha kiwanda cha mbao ambapo miti ya asili kama mipingo, mikongo na mininga ilikatwa. Wananchi wa vijiji vinne vilivyotoa sehemu ya ardhi yake ambavyo ni Mavuji, Liwiti, Migeregere na Nainokwe walikosa sehemu za kulima na kwa wale waliopata ajira walikaa muda mrefu bila mishahara na mwisho mwekezaji aliamua kutelekeza ardhi akatoroka bila kuwalipa stahiki zao.

Kutokana na mifano hiyo, ni dhahiri kwamba uwekezaji mkubwa umeleta athari za wazi kabisa kwa wananchi wa kawaida hasa wanavijiji wanaotumia ardhi kujikimu. Kikubwa zaidi, sehemu kubwa ya wawekezaji ambao hawajazingatia taratibu za kupata ardhi na wale wanaoitumia kwa kukodisha, wamechangia kuwepo kwa migogoro baina yao na wanachi wa maeneo husika kwa kuwa wananchi wanatamani kumiliki na kutumia ardhi ambayo wawekezaji wamehodhi na kuwakodishia wananchi kwa gharama kubwa.

Hivyo basi, ni vema serikali ikabatilisha umiliki wa ardhi kwa wawekezaji waliopata ardhi kinyume cha taratibu na kuigawa kwa wananchi wasio na ardhi ili kupunguza migogoro inayotokana na uhaba wa ardhi. Pia, iwachukulie hatua viongozi wote wanaokiuka taratibu za ugawaji wa ardhi ikiwa ni pamoja na viongozi wa vijiji wanaogawa ardhi bila idhini wala ridhaa ya wananchi kupitia mikutano mikuu ya vijiji

» Inatoka uk. 1

wananchi na wanyamapori katika maeneo ya Hifadhi za Taifa tofauti na mfumo uliokuwepo. Baada ya Uhuru, serikali ya Tanganyika iliendelea kupanua maeneo ya hifadhi za wanyamapori kwa kufikisha Hifadhi za Taifa tatu, mapori ya akiba tisa na kuanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Upanuzi huu uliendelea hadi katika maeneo ambayo wananchi walikuwa wakiyatumia kwaajili ya shughuli zao za kiuchumi kama vile Kilimo, Ufugaji, uvuvi, uwindaji na urinaji wa asali. kwavile msingi wa uhifadhi ulijengwa katika dhana ya kutenganisha maisha ya binadamu na wanyamapori, wananchi waliendelea kupoteza maeneo yao kila hifadhi mpya ilipoanzishwa au ya zamani kuongezwa mipaka yake. Mwaka 1974, ilitungwa sheria ya wanyamapori ambayo ilitumika hadi mwaka 2009 sheria mpya ya wanyamapori ilipotungwa. Sheria hii mpya ilitungwa ili kuwianishwa na sera ya Wanyamapori ya 1998 iliyoleta dhana mpya ya uhifadhi wa wanyama kwa kuruhusu hifadhi za Wanyama Pori za jamii (WMA) .

Hadi kufikia mwaka 2014 idadi ya Hifadhi za Taifa zimeongezeka kufikia kumi na sita (16). Nyingi ya hifadhi hizo zimeanzishwa au kupanuliwa kwa kumega ardhi za vijiji na hivyo kuathiri haki za ardhi za wananchi waliokuwa wakiitumia ardhi hiyo kwa matumizi mbalimbali. Baadhi ya hifadhi ambazo uanzishwaji au upanuzi wake umeibua malalamiko makubwa ni pamoja na; Mkomazi (km 3,245), Saadani (km 1,100), Ziwa Manyara (km 330), Tarangire (2,850), Ruaha (20,226) na Serengeti (14 (763). Kwa mfano, hifadhi ya Ruaha ambayo ni kubwa kuliko zote nchini ilipanuliwa mwaka 2008 kwa kuongezewa maeneo yaliyokuwa pori tengefu la Usangu na baadhi ya maeneo yaliyokuwa vijiji vya bonde la Usangu na hivyo kuongezeka ukubwa wake hadi kufikia kilomita za mraba 20,226.

NI JUKUMU LETU SOTE KUHAKIKISHA KUWA WANYAMAPORI NA MAPORI YAO YANALINDWA KWAAJILI YA VIZAZI VYA SASA NA VIJAVYO.

## Athari za upanuzi wa maeneoya hifadhi za wanyamapori kwa wakazi wa maeneo jirani.



*Wanyama aina ya Tembo katika Hifadhi ya Taifa Tarangire*

Aidha, upanuzi ama uanzishwaji wa maeneo hayo ya hifadhi umekuwa ukiambatana na ukiukwaji wa haki za binadamu kama vile uchomaji moto au ubomoaji wa makazi, uharibifu wa mazao na ulipwaji wa fidia ndogo isiyoendana na viwango halisi vya thamani ya mali wanazopoteza. Mfano halisi ni kwa wananchi wa Loliondo wanaoishi kwenye vijiji vinavyopakana na pori tengegu la Loliondo ambao mwaka 2009 walichomewa nyumba na mazao yao na kusababisha takribani wakazi 10,000 wa vijiji nane kukosa mahali pa kuishi na kupotelewa na mifugo yao katika jitihada za kujiokoa eneo la hifadhi likipanuliwa. Katika tukio hili ndugu Ngodidyo Rotiken alipoteza jicho lake kutokana na kipigo cha walinzi wa mamlaka za hifadhi huku mama mmoja akisadikiwa kupoteza ujauzito.

Wananchi wanaoishi maeneo ya hifadhi wameendelea kuathirika na mabadiliko ya sheria ya wanyamapori ya mwaka 2009 ambayo yametenga mapori tengefu kutoka kwenye ardhi ya vijiji. Baadhi ya maeneo yaliyokumbwa na migogoro ya aina hiyo ni pamoja na; Loliondo, Ulanga, Kilombero, Mbarali, Rufiji na Simanjiro.

Licha ya ukweli kuwa wanyamapori wanaliingizia taifa fedha nyingi za kigeni kutokana na shughuli za kitalii na uwekezaji katika sekta hii, ni dhahiri pia kuwa wananchi wanaoishi karibu na maeneo yenye hifadhi hizo wanapaswa kupewa kipaumbele kwa kutambua na kulinda haki zao pamoja na kuweka mipango madhubuti ya kuhakikisha kuwa wananufaika na shughuli za uhifadhi kwa ujumla. Ili hayo yawezekane, serikali haina budi kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi nchi nzima ili kutambua na kuainisha ukubwa na aina ya matumizi katika kila kijiji, kudhibiti uvamizi wa ardhi za vijiji na kutoa hati miliki za kimila kuwawezesha wananchi kunufaika na haki zao.

Hali kadhalika, ni vema haki ya kumililki ardhi ikapewa ulinzi zaidi kwa kuingizwa katika katiba ya Jamhuri ili wamiliki na watumiaji wa ardhi wawe na uhakika katika milki ya ardhi na matumizi ya rasilimali zilizomo.

Ni vema pia kuwawezesha wananchi kupata baadhi ya huduma za msingi kama vile maji, na malisho hasa wakati wa kiangazi kwa jamii za wafugaji ili kuepusha mwingilino wa matumizi katika makundi mengine ya ardhi na kusababisha migogoro.

# JE MPANGO WA MATUMIZI YA ARDHI UNA NAFASI GANI KATIKA KUPUNGUZA MIGOGORO YA ARDHI NCHINI?

*Na. Joseph Chiombola*

Moja ya sababu ambazo Wizara ya ardhi pamoja na watafiti wengi wamekuwa wakizitoa kuhusiana na kukithiri kwa migogoro ya ardhi nchini ni kasi ndogo ya upangaji wa ardhi mijini na vijijini kulingana na matumizi yake. Sababu hiyo ndio pia ilitoa msukumo wa kutungwa kwa sheria ya mipango ya matumizi ya ardhi namba 6 ya mwaka 2007. Sheria hii imetafsiri, Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Kijiji kuwa ni utaratibu wa kutathmini na kupendekeza namna mbalimbali za matumizi ya maliasili/rasilimali ili kuinua hali ya maisha ya watumiaji ardhi.

Tangu kutungwa kwa sheria hii, kumekuwa na jitihada za wadau mbalimbali kusaidia uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi hususan vijijini kwa malengo tofauti. Hata hivyo, ili kuhakikisha kuwa wanakijiji wanashiriki kikamilifu, ni muhimu kuzingatia makundi mbalimbali yaliyopo katika kijiji ambayo yana utashi na malengo yanayotofautiana. Hii itaepusha migogoro ya ardhi ambayo licha ya kuwepo kwa sera, sheria, kanuni na vyombo mbalimbali vya usimamizi na utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini bado migogoro hiyo inaendelea kuzikabili jamii nyingi za watanzania hasa waishio vijijini. Kwa siku za karibuni, utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji unaelezwa kuwa ni njia mojawapo madhubuti ya kukabiliana na migogoro ya ardhi.

Kwanza, mipango ya matumizi ya ardhi husaidia usimamizi wa ardhi iliyotengwa na kupangwa kwa matumizi mahususi, huepusha mwingiliano kati ya mtumiaji mmoja na mwingine, huwezesha kuwepo kwa matumizi endelevu kwa kuzingatia sheria ndogondogo zilizotungwa na husaidia kuhifadhi mazingira hususan vyanzo vya maji na misitu.

Pili, mipango ya matumizi ya ardhi huwapa alama ya utambulisho wamiliki wa ardhi kupitia vyeti vya hatimiliki za kimila. Hata ukitokea mgogoro unaohitaji uthibitisho wa umiliki ni rahisi kwa mwenye hati hii kuitumia kama kielelezo cha ushahidi wake mbele ya vyombo vya haki hususan mabaraza ya ardhi.


Tatu, mpango hutoa fursa kwa wafugaji na wakulima kupata maeneo ya malisho na kilimo, hivyo kuepusha migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo husababishwa na kugombea rasilimali hizo hasa wakati wa ukame. Kwa kufuata mpango huo wakulima wataweza kutumia mbinu za kisasa katika kilimo na wafugaji kukabiliana na ukame ambao huathiri maeneo yao ya asili. Mpango wa matumizi ya ardhi utasaidia kupunguza migogoro ya kugombea maeneo ya malisho na kilimo, vyanzo vya maji na kusaidia matumizi endelevu ya ardhi husika. Mifano hai ya vijiji vilivyotenga maeneo ya ufugaji na njia za mifugo kukabiliana na migogoro ya ardhi ni pamoja na Kihesa Mgagao wilayani Kilolo na Magunguli cha Wilaya ya Mufindi vyote ya mkoa wa Iringa.



*Mpango wa matumizi ya ardhi kijiji cha Magunguli Mufindi*

Nne, suala la ushirikishwaji wa wananchi ni muhimu sana. Migogoro ya ardhi itapungua na pengine kwisha kabisa endapo mipango ya matumizi ya ardhi itafanyika kwa mujibu wa sheria yaani kwa kufuata hatua na kushirikisha wananchi ambao ni walengwa wa mipango hiyo.

Pamoja na kuwa utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ongezeko ya watu na mifugo, mabadiliko ya hali ya hewa yanayosababisha wananchi kuhamahama na ufinyu wa fedha za bajeti inayopangwa ili kuwezesha utekelezaji wa mipango hiyo kwa wakati, serikali ikiweka dhamira ya kweli katika kuhakikisha wananchi wake wanapata uhakika wa milki ya ardhi kwa njia ya kupima na kupanga matumizi ya maeneo hususan ardhi za vijiji, suala la uhaba wa fedha litaonekana dogo kwani serikali itaipa kipaumbele sekta ya ardhi na kuipangia fedha za kutosha katika bajeti ili kukabiliana na migogoro ya ardhi ambayo imezidi kuleta athari kubwa kwa taifa.



*Vailet Sanga wa kijiji cha Kihesamgagao Wilayani Kilolo-akipokea Hatimiliki yake ya kimila.*

# MIGOGORO YA ARDHI INAHITAJI SULUHU YA KUDUMU

*Na: Nakamo Tenende*



Hakuna ubishi kwamba ardhi ni rasilimali muhimu na ya kipekee kwenye maisha ya wananchi na taifa la Tanzania kama ilivyo chanzo cha uhai na maisha yao endelevu. Ardhi ndilo chimbuko la uzalishaji mali wa aina zote, uhifadhi wa maliasili na mazingira, uoto asili na baoanuai pamoja na utajiri wa asili ulio chini ya uso wa nchi kama vile mafuta na gesi asilia.

Hata hivyo, Tanzania imegubikwa na migogoro ya ardhi kwa takribani kila kundi. Migogoro hii inawazuia wananchi kunufaika na rasilimali hii adhimu kupitia shughuli zao za uzalishaji mali kama vile kilimo, ufugaji, uchimbaji madini, uokotaji wa matunda na biashara mbalimbali zinazoendeshwa katika ardhi. Ipo migogoro kati ya Wakulima dhidi ya wafugaji, wakulima kwa wakulima, wachimbaji wadogo dhidi ya wakubwa, wawekezaji dhidi ya wananchi walio kando ya maeneo ya uwekezaji, mamlaka za hifadhi dhidi ya wakazi wa maeneo ya pembezoni mwa hifadhi na makundi mengine yenye maslahi katika ardhi.

Jitihada za kutatua migogoro hii zimeanza muda mrefu lakini hazijazaa matunda. Kwa mfano, sheria ya mabaraza na mahakama za ardhi ya mwaka 2002, ilianzishisha mabaraza ya ardhi ya vijiji kwa lengo la kuwezesha usuluhishi baina ya wananchi wa ngazi ya vijiji sambamba na mabaraza ya Kata ambayo nayo yamekuwepo kwa muda mrefu tangu mwaka 1985. Hata hivyo, mabaraza haya kwa muundo na mfumo wake, yameshindwa kuwa suluhu ya migogoro maana wajumbe wake hawana uwezo wa kuhimili vishindo vya migogoro mipya inayoibuka hasa kuhusiana na uwekezaji. Kwa ujumla, mfumo na muundo wa mabaraza ya ardhi haujasaidia kutatua migogoro kama ilivyokusudiwa.

Yapo mengi yanayoweza kufanyika ili kukabiliana na migogoro ya ardhi na kupata suluhu ya kudumu. Kwanza, bajeti ya wizara ya ardhi na idara zake katika halmashauri iongezwe. Kwa takribani miaka mitano sasa, kilio cha wizara ya ardhi kila ikiwasilisha bajeti yake huwa ni kiasi kidogo cha fedha za maendeleo kuiwezesha kutekeleza majukumu yake. Kwa wastani, Wizara imekuwa ikipata kati ya bilioni 40 na 50 kwa mwaka isipokuwa kama kuna mradi maalumu kama ule wa ujenzi wa mji mpya wa Kigambini ambapo wizara iliwahi kuomba bilioni 101 mwaka 2013. Hata hivyo fedha hizo licha ya kuidhinishwa na Bunge huwa hazitolewi zote.

Ni dhahiri kwamba wizara ikipata mgawo wa kutosha wa bajeti ya taifa, itajielekeza katika kukabiliana na changamoto za upimaji na usimamizi wa ardhi na hivyo kuwezesha wananchi kuwa na uhakika wa milki zao pamoja na makazi.

Pili, upimaji wa ardhi yote ya mijini na vijijini utapunguza migogoro ya ardhi hasa inayotokana na ugawaji wa hati pandikizi pamoja mwingiliano wa kimatumizi baina ya watu wawili au makundi zaidi ya moja. Inashangaza kuona kuwa hadi sasa eneo la nchi liliopimwa halizidi asilimia 10 kati ya zaidi ya eneo la nchi lenye ukubwa kwa kilometa za mraba 945,087.

Tatu, ugatuzi wa madaraka ya usimamizi wa Ardhi kwenda kwenye vyombo vyenye usimamizi na ushiriki wa wananchi moja kwa moja kama vile Halmashauri za Vijiji na Mikutano Mikuu ya Vijij, utasaidia wananchi kushiriki kwenye maamuzi yanayowahusu hasa kuhusiana na milki na matumizi ya ardhi.

Nne, ni lazima kuzingatia haki na maslahi ya wenyeji wakati wa michakato ya kuwapatia wawekezaji ardhi kwa ajili ya uwekezaji mkubwa kwenye ardhi za vijijini. Inapolazimu kuwahamisha wanavijiji kwa miradi ya maendeleo ya kitaifa, wanapaswa kulipwa fidia kamili, ya halali na kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuwapatia maeneo mbadala ya makazi na kilimo au ufugaji.

Mwisho kabisa ni kuepukana na siasa za vyama wakati wa kutafuta suluhu ya migogoro ya Ardhi. Mara kadhaa wananchi kwenye maeneo ya migogoro ya Ardhi wamekuwa wakilalamikia wanasiasa katika nafasi zao kama viongozi wamekuwa wakitoa ahadi za kutatua migogoro ya wananchi bila kusuluhisha migogoro hiyo hasa unapokaribia wakati wa uchaguzi. Wananchi huhadaika wakidhani ahadi za wanasiasa zina tija kuliko utaalamu wanaoelekezwa. Hatimaye uchaguzi ukipita, inakuwa vigumu kupata suluhu maana ahadi nyingine zinakuwa zilitolewa kisiasa tu.

# Wananchi wanasemaje JUU YA MIGOGORO YA ARDHI

*Na. Gloria Jimwaga*

## Ufinyu wa bajeti katika sekta ya ardhi utazamwe kwa umakini.



Mara nyingi nimesikia kuwa miradi katika sekta ya ardhi inayohusu upimaji wa viwanja, mashamba, uanzishwaji wa mabaraza ya ardhi, utoaji wa mafunzo kwa viongozi na wananchi juu ya sheria za ardhi imekuwa haitekelezeki kutokana na ufinyu wa bajeti. Mimi ninavyofahamu ardhi ina umuhimu wa kipekee kwa kila mtanzania hivyo inapaswa kupewa kipaumbele hata katika bajeti. Naomba serikali ihakikishe kuwa Wizara ya Ardhi, Halmashauri za Wilaya na taasisi nyingine zinazotusaidia kama hii yenu zinapewa bajeti ya kutosha ili kuhakikisha kuwa rasilimali hii inasimamiwa na kutumiwa ipasavyo kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo.

**MARIAM SELEMAN**
*Mkiti Kijiji Mipeko – Mkuranga Pwani*



## Mabaraza ya ardhi ya vijiji yaboreshwe

Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji yana umuhimu wake katika utatuzi wa migogoro ya ardhi maana yako katika ngazi ya msingi kabisa kijijini. Mabaraza haya yanatoa fursa ya wanavijiji kuwa huru katika kutatua migogoro yao ya ardhi kutokana na wajumbe wake kuwa wananchi wa kawaida katika kijiji husika. Changamoto kubwa inayokabili mabaraza haya ni kukosekana kwa mafunzo kwa wajumbe wanaounda mabaraza haya ili wawe na utambuzi wa sheria za ardhi pamoja taratibu zinazotumika katika utatuzi wa migogoro ya ardhi. Dosari hiyo ikiondoka basi migogoro itakuwa historia vijijini maana mabaraza yatafanya kazi kama yalivyokusudiwa.

**AMIRI MATAMBO**
*Mkiti/Kijiji Mkerezange - Mkuranga*

## Ulimbikizaji wa ardhi unachochea migogoro ya ardhi vijijini.

Katika vijiji tunavyoishi wawekezaji wamekuwa wakinunua ardhi kubwa kutoka kwa wananchi ambayo hatimaye hawawezi kuiendeleza kwa wakati. Kushindwa kuiendeleza ardhi kumekuwa kukisababisha wanavijiji wasiokuwa na ardhi za kilimo na makazi kuvamia mashamba hayo hali inayozua migogoro ya ardhi. Katika kijiji cha Vikindu wilayani Mkuranga kuna mwekezaji anayemiliki ardhi yenye ukubwa wa takribani ekari 200 lakini ameshindwa kuliendeleza eneo hilo kwa muda mrefu. Eneo hili limekuwa likizua migogoro ya mara kwa mara kutokana na wanavijiji kulivamia.

Nitoe ushauri kwa serikali kuwa kuna umuhimu wa kuboresha sera na sheria za ardhi ili kuhakikisha kuwa kila mwekezaji anayepewa ardhi kijijini anakuwa na uwezo wa kuiendeleza na pale anaposhindwa hatua za haraka za kisheria zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kumnyang'anya ardhi husika na kugawiwa kwa watu wenye uwezo wa kufanya maendelezo yenye tija kwa wananchi na taifa.



**RAJABU MEDE**
*M/Kiti Kijiji Vikindu - Mkuranga*



*kundi la ng'ombe magunguli mufindi*

# WAJIBU NA MAMLAKA YA MABARAZA YA UTATUZI WA MIGOGORO

*Baraza hili, ni chombo cha usuluhishi tu si cha hukumu, hutumia mila, desturi na taratibu za usuluhishi wa migogoro katika kijiji, huitisha vikao vya kusikiliza madai ya migogoro kutoka kwa walalamikaji na kujitahidi kuwapatanisha.*

Katika toleo hili, kona ya sheria inaangazia muundo na mamlaka ya vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi. Vyombo hivi vinaundwa kwa mujibu wa sheria ya mabaraza na mahakama za ardhi namba 2 ya 2002. Vyombo hivyo ni Baraza la ardhi la Kijiji, Baraza la Kata, Baraza la Ardhi na nyumba la Wilaya, Mahakama kuu na Mahakama ya Rufaa. Katika toleo hili, tunachambua mabaraza ya ardhi ya vijiji na mabaraza ya kata.

### BARAZA LA ARDHI LA KIJIJI

Huundwa na wajumbe 7 kati yake wanawake wasipungue 3. Wajumbe huteuliwa na Halmashauri ya kijiji na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu, hukaa madarakani kwa miaka 3, na huweza kuchaguliwa tena kwa miaka 3 tu. Sifa za wajumbe lazima awe raia, mwanakijiji, kuanzia miaka 18, awe na akili timamu, asiye kiongozi katika kijiji na awe mwadilifu. Baraza hili, ni chombo cha usuluhishi tu si cha hukumu, hutumia mila, desturi na taratibu za usuluhishi wa migogoro katika kijiji, huitisha vikao vya kusikiliza madai ya migogoro kutoka kwa walalamikaji na kujitahidi kuwapatanisha. Baraza halina



uwezo wa kutoza faini, kuweka kizuizini, kugawa ardhi ya kijiji, kumnyima mtu haki kwa kigezo cha jinsia, umri, rangi au kabila, na kutoa hukumu bali husuluhisha tu.

### BARAZA LA KATA

Huundwa na wajumbe wasiopungua 4 na wasiozidi 8 kati yao wanawake wasipungue 3. Wajumbe huchguliwa na kamati ya maendeleo ya Kata toka vijiji vya kata husika, hudumu kwa miaka 3 wanaweza kuchaguliwa tena kwa miaka 3 tu. Sifa za wajumbe zinafanana na za wajumbe wa Baraza la ardhi la Kijiji.

Baraza la Kata husikiliza mashauri yasiyozidi kiwango cha ukomo wa fedha wa milioni 3 ndani ya kata husika. Lina uwezo wa kutoa amri za kimahakama kama vile kuagiza urejeshwaji wa ardhi iliyonyang'anywa, kumtaka mtu atimize wajibu wake ndani ya mkataba, kutoa amri au maagizo ya kisheria, kuagiza ulipaji wa gharama zitakazokuwa zimetumiwa na atakayeshinda kesi au mashahidi wake na kutoa agizo lolote ambalo litakuwa la haki kwa hukumu itakayotolewa.

### HITIMISHO

Mfumo wa mabaraza ulianzishwa ili kutoa fursa kwa wananchi kuifikia milango ya haki kuanzia ngazi ya msingi kabisa. Endapo mfumo huu utaimarishwa na maamuzi yakatekelezwa kwa mujibu wa sheria basi unaweza kusaidia kupunguza migogoro mingi ya ardhi nchini bila kuathiri mifumo ya maisha na uzalishaji mali hasa kwa wananchi wanaotegemea rasilimali ardhi kuendesha maisha yao.

BARAZA LA KATA HUSIKILIZA MASHAURI YASIYOZIDI KIWANGO CHA UKOMO WA FEDHA WA MILIONI 3 NDANI YA KATA HUSIKA.



*FemAct wakiwa katika jitihada za usuluhishi wa mgogoro wa ardhi Loliondo*




*Moja ya mitambo ya uchimbaji madini ya dhahabu ukiwa kazini*

# UGUNDUZI WA GESI ASILIA UWE CHACHU YA MAENDELEO KWA WANANCHI BADALA YA KUIBUA MIGOGORO MIPYA

***Faida kubwa inayotajwa kuhusishwa na wananchi hasa fursa za ajira ni kuanzishwa kwa viwanda vya mbolea kutokana na mabaki ya usindikaji wa gesi asilia kwa ajili ya matumizi.***

*Na; Yefred Myenzi*

Tanzania imebahatika kuwa na rasilimali za asili kama vile madini, wanyamapori na misitu ambayo kwa nyakati tofauti imekuwa ikivutia wawekezaji toka sehemu mbalimbali duniani. Hata hivyo, uwekezaji wa kutoka nje katika sekta za madini na wanyamapori umekuwa ukipigiwa kelele kuwa unawaathiri wananchi wanaoishi pembezoni mwa maeneo yenye rasilimali hizo badala ya kuwa chachu ya maendeleo yao.

Katika taarifa yao ya utafiti iliyotolewa mwaka 2010 kuhusu namna Tanzania inavyopoteza mapato katika sekta ya madini kwa njia za ukwepaji wa kodi, misamaha ya kodi na motisha nyingine kwa wawekezaji wakubwa; watafiti Mark Curtis na Tundu Lisu walionyesha kuwa uwekezaji mkubwa katika sekta ya madini umekuwa pia chimbuko la migogoro ya ardhi baina ya wawekezaji na wananchi wa maeneo husika. Taarifa hiyo ambayo ilichapishwa na jumuiya za kidini nchini yaani BAKWATA, CCT na TEC, inatoa mfano kuwa kati ya mwaka 1996 na 1998 ilipoendeshwa operesheni ya kuondoa wachimbaji wadogo ili kupisha uanzishwaji wa mgodi mkubwa wa Bulyanhuru, wananchi takribani 400,000 waliokuwa wakitegemea uchimbaji na shughuli zinazoendana na uchimbaji dhahabu walipoteza shughuli zao huko Kahama. Watu hao wote walitawanyika kusikojulikana na huenda walienda kusababisha maafa mengine mbele ya safari kutokana na kukosa maeneo ya kuendeshea maisha yao na hata kukosa fidia kwa mali walizopoteza.

Hali kadhalika, wananchi wa Geita ambako mgodi mwingine wa dhahabu ulianzishwa, walitolewa katika maeneo yao kupisha uwekezaji mkubwa huku wakisubiri hatima yao mahakamani lakini wameishi kwa miaka zaidi ya kumi katika mahema na vibanda vya muda wakisubiri haki inayochelewa kupatikana. Katika eneo jingine la uchimbaji mkubwa wa dhahabu la North Mara huko Tarime, wenyeji wa maeneo yanayozunguka mgodi wamekuwa katika mahangaiko makubwa ya kupambana na mwekezaji aliyedaiwa kutiririsha maji yenye sumu kwenye mto Tigiti unaotumiwa na wananchi kwa matumizi ya kawaida ya kuendeshea maisha yao ya kila siku. Licha ya taarifa mbalimbali za kitafiti kuonyesha athari za utiririshaji huo hadi kuilazimu kamati ya Bunge ya ardhi, maliasili na mazingira kufanya ziara katika eneo hilo, bado hali ya utiririshaji maji hayo iliendelea kwa takribani miaka mitatu (2010-2012) ingawa sasa kuna taarifa kuwa umefanyika udhibiti wa kutosha.

Wakati tukiyatafakari madhila hayo yote ambayo baadhi yake hayajapata suluhu, Tanzania imegundulika kuwa na kiasi kikubwa cha gesi asilia inayokadiriwa kufikia kiwango cha futi za ujazo trillion 46 sawa na takribani lita trillion 566.25 za ujazo. Ugunduzi huu umefanywa na makampuni ya kigeni yakiwemo kampuni ya stateoil ya nchini Norway na mshirika wake ExxonMobil ambao wote kwa pamoja ni wabia wa shirika la maendeleo ya mafuta nchini TPDC. Makampuni haya ambayo yamekuwepo nchini kuanzia miaka ya 2005 na kuendelea, yanaendelea

na utafiti sambamba na uchimbaji katika maeneo ambayo ugunduzi umekamilika yakiwemo maeneo ya kina kirefu cha bahari ya Hindi.

Taarifa za kitaalamu zinaonyesha kuwa gesi iliyopo nchini inaweza kuchimbwa kwa zaidi ya miaka mia moja ambao si muda mfupi hata kidogo kwa uhai wa taifa na mustakabali wa maendeleo yake. Inaelezwa kuwa gesi asilia inapatikana kwa wingi kwenye kina kirefu cha Bahari ya Hindi ukanda wa pwani ya Mtwara na katika visiwa vya Songosongo katika mkoa wa Lindi. Yapo maeneo mengine pia yanayotajwa kuwa na kiwango kikubwa cha gesi yakiwemo Mnazibay na Mkuranga mkoa wa Pwani.

Tofauti na madini ambayo hata uchorongaji wake tu hufanyikia nje ya nchi kutokana na kile kinachoelezwa kuwa nchi yetu haina mitambo ya kuchenjua na kuchoronga madini na vito, gesi asilia itaandaliwa kwa kiasi cha kutumika hapa hapa nchini. Licha ya matumizi ya viwandani, gesi asilia inaelezwa kuwa ni chanzo bora cha nishati ya majumbani kwa ajili ya kupikia. Pia hutumika kama nishati katika magari na mitambo mbalimbali. Faida kubwa inayotajwa kuhusishwa na wananchi hasa fursa za ajira ni kuanzishwa kwa viwanda vya mbolea kutokana na mabaki ya usindikaji wa gesi asilia kwa ajili ya matumizi.

Waziri mwenye dhamana ya Nishati na Madini amekuwa msitari wa mbele kuelezea kuwa ugunduzi, uchimbaji na matumizi ya gesi asilia ndio utaipaisha Tanzania kiuchumi kutoka hali ya sasa na kuwa nchi ya uchumi wa viwanda katika miaka kumi ijayo. Kwa kweli, watanzania lazima tujivunie fursa hii ya kugunduliwa kwa gesi na kuichukulia kama nafasi ya kutimiza ndoto kubwa anazoota mheshimiwa waziri. Hata hivyo, ili kufikia kwenye uchumi wa aina hiyo ni lazima mambo makubwa manne ya msingi yafanyike.

Kwanza, wananchi washirikishwe katika hatua zote za maendeleo ya utafutaji, uchimbaji na matumizi ya gesi. Hatua hii itasaidia kuweka uwazi katika uwekezaji ambao mara nyingi ndicho kimekuwa kichocheo cha migogoro. Kwa mfano, serikali imeweka bayana kuwa ili gesi hiyo iwe na matumizi yenye tija kwa taifa, itabidi kusafirishwa kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam kwa bomba lenye urefu wa km 538. Ni dhahiri kwamba kwa umbali huu, wapo watu ambao maeneo yao yataingiliwa ili kuruhusu bomba lipite na watahitaji fidia. Ulipwaji wa fidia kamili, ya haki na kwa wakati ni jambo ambalo mara nyingi limekuwa likiibua migogoro kutokana na usiri na udogo wa wango vya fidia. Ni vema kwa miradi ya gesi ambayo inakuja baada ya nchi kupata uzoefu kutokana na miradi ya madini ilivyoelezwa hapo awali, kukawa na uwazi mkubwa ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

Pili, ziwekwe fursa maalumu za uwezeshaji kwa wananchi wa maeneo husika. Kuna usemi wa wahenga usemao hisani huanzia nyumbani. Ni vema wananchi wa maeneo husika wakapewa kipaumbele katika ajira na utoaji wa huduma ili pato litokanalo na fursa hizo liwanuifaishe wenyeji wa maeneo hayo angalau yafanane na hadhi ya uwekezaji husika. Uzoefu umeonesha kuwa maeneo yenye uwekezaji mkubwa hasa wa madini na wanyamapori kama vile Bulyanhulu, Geita, Nzega, North Mara pamoja na Loliondo bado yako katika umaskini licha ya kuzalisha utajiri mkubwa kwa wawekezaji.

> KWANZA, WANANCHI WASHIRIKISHWE KATIKA HATUA ZOTE ZA MAENDELEO YA UTAFUTAJI, UCHIMBAJI NA MATUMIZI YA GESI.

Tatu, serikali inapaswa kuweka utaratibu ambao utawawezesha wananchi kuwa wabia wa makampuni yanayowekeza katika maeneo husika kwa kutenga kiwango cha hisa ambacho wananchi kupitia vikundi vyao mbalimbali wanaweza kushiriki kwenye uwekezaji. Endapo hili linakuwa gumu kwa makampuni, serikali inaweza kuweka mfumo wa kisheria utakaoyalazimu makampuni yanayowekeza kutenga asilimia fulani ya pato lake kwa ajili ya kusaidia shughuli za maendeleo ya maeneo husika. Tumezoea kuona makampuni yakifanya hisani ya kurudisha kwa jamii lakini jambo hilo hufanyika kwa hiyari na hisani ya mwekezaji na asipofanya hivyo habanwi na sheria yoyote. Lakini kukiwa na utaratibu wa kisheria unaolindwa na mkataba maalumu, watawajibika kurejesha kwa jamii na tutashuhudia maendeleo ya kasi katika maeneo yaliyojaliwa kuwa na rasilimali hizi.

Nne, mikataba ya gesi iwe wazi, ijadiliwe na kuridhiwa na bunge la Jamhuri ambalo lina wawakilishi wa wananchi ili kuhakikisha kuwa maslahi ya taifa yamezingatiwa katika kila kipengele cha mkataba husika. Hili pia linatokana na uzoefu wetu katika sekta ya madini ambako tumeshuhudia mikataba mibaya inayoinyima nchi mapato ya uhakika licha ya kurekebishwa kwa sheria ya madini mwaka 2010. Baadhi ya mikataba ya madini ikiwemo iliyosainiwa nje ya nchi kwa kisingizio cha kuogopa kupoteza fursa za uwekezaji imeendelea kulinyima taifa mapato ya uhakika kwavile kuna vipengele visivyorekebishika hata baada ya sheria kurekebishwa. Endapo mikataba ya gesi asilia itakuwa siri tena, si ajabu tukarudia makosa yale yale yaliyofanywa katika sekta ya madini. Ni dhahiri kwamba mikataba mizuri italinda maslahi ya wananchi wa maeneo husika na kuwezesha pato linalotokana na rasilimali hizo muhimu kuingia katika hazina ya taifa kuwanufaisha watanzania.

Rai yetu kama ilivyokuwa kwa sekta ya madini ni kuwa, utajiri huu mkubwa usigeuke kuwa laana kwa wananchi wanaoishi maeneo yenye rasilimali hiyo adhimu bali uwe chachu ya mabadiliko ya maisha yao kuwa bora. Maeneo kama Mtwara na Lindi, yamekuwa nyuma kimaendeleo kulinganisha na maeneo mengine hususan kwa sekta za miundombinu na huduma za jamii kama vile umeme, shule na hospitali. Licha ya kuwepo umuhimu wa gesi iliyogunduliwa kunufaisha watanzania katika ujumla wao, ni lazima iwekwe mipango madhubuti ya kuhakikisha kuwa wenyeji wanakuwa sehemu ya mabadiliko yanayotokana na rasilimali ya gesi iliyogunduliwa badala ya kuwa mashuhuda wa mabomba yanayopitisha gesi kwenda kwingineko huku wao wakibaki katika hali sawa na za wenzao wa Bulyanhulu, Nzega, Geita, North Mara na Loliondo.

# ARDHI NI UHAI

HAKIARDHI ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 12 MEI - AGOSTI 2014



*Mh. Joseph Mhumba, M/kiti wa H/wilaya ya Kilolo (wa 4 kati) katika picha ya pamoja na wananchi waliopata hatimiliki za kimila - Kihesamgagao Iringa*

## BAADHI YA MACHAPISHO

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ardhi ni Uhai 1995 | Georgis Hadjiyavanis |
| 2. | Not yet Democracy: Reforming Land tenure in Tanzania 1998 | Issa G. Shivji |
| 3. | Haki za Wamasai waishio Ngorongoro 1999 | Issa.G Shivji/Wilbert Kapinga |
| 4. | Mwongozo wa haki za Ardhi kwa wananchi wa Tanzania 2002 | Issa G.Shivji/Deus Kibamba |
| 5. | Silencies in NGOs Discourse Occasional paper No.1 2006 | Issa G.Shivji |
| 6. | The mute Plunder "Bioreosurces and disposesion in Tanzania 2008 | Ng'wanza Kamata |
| 7. | Public Perceptions on bioresources conservation in Tanzania 2008 | HAKIARDHI |
| 8. | Accumulation by land dispossession and labor devaluation 2011 | HAKIARDHI |
| 9. | Biofuels in Tanzania 2013 | HAKIARDHI |
| 10. | Local people's perception on climate change in Tanzania 2013 | Cathbert Tomitho |
| 11. | Land grabbing in a post investment Rufiji basin 2013 | Mwami&Kamata |
| 12. | Ardhi iwe nguzo katika katiba mpya 2014 | HAKIARDHI |